


Text and illustrations: Willem de Vink


YESU MASIHA



NINI NI...




Baraka: Ni vitu vyote vizuri amba-yo Mungu anataka kuwapa watu wale amba-o wanafanya kila ana-chotaka.




Biblia: Katika Biblia unaweza kusoma jinsi Mungu anavyowaan-galia watu na jinsi anavyohusika nao.



Dhambi: Mambo tuyafanyayo kinyume na mapenzi ya Mungu ambayo hutuzuia sisi kufikia mpango wa Mungu alio nao kwa ajili yetu (ukurasa wa 4).



Imani: Kumwamini Mungu kwa kile alichoahidi kukifanya (ukurasa wa 58).



Kurudi: Kila kitu kitakuwa kipy-a wakati Yesu atakaporudi ulimwen-guni. Mbingu na nchi zitaba-dilishwa na Mungu (ukurasa wa 57).



Malaika: Mjumbe wa Mungu asiyeonekana (ukurasa wa 5).

Maombi: Unaongea na Mungu, kimya au kwa sauti na unamsikili-za yeye (ukurasa wa 18, 19 na 42).

Masiha: Mfalme 'Mpakwa Mafuta'. Masiha (neno la Kiebrania) lime-tafsiriwa kwa Kigiriki kama Kristo (ukurasa wa 52 na 55).

Msalaba: Chombo cha mateso am-bacho kilitumika kumsulubisha Yesu kwa hiari yake mwenyewe. Imekuwa ni ishara kwa wafuasi wote wa Yesu (ukurasa wa 25 na 50).

Msamaha: Mungu husamehe, inga-wa hakuna mtu anayestahili. Mungu husamehe kama kweli wewe umetu-bu dhambi na unataka kubadilika. Msamaha unapatikana kwa sababu Yesu alichukua adhabu zetu ambazo sisi tulistahili (ukurasa wa 58).

Mtume: Mfuasi wa Yesu (ukurasa wa 18).

Mwana wa Mungu: Jina la Yesu. Ni Mungu aliyejuja duniani kama mwanadamu, kama Mwana wa Mungu.

Pasaka: Ni sherehe ya kufufuka kwa Yesu. Kwa asili yake, sherehe hiyo ilikuwa sherehe ya kukumbuka ukombozi wa Waisreali kutoka Misri. Sherehe hiyo iliitwa Pasaka pia (ukurasa wa 38-54).

Roho Mtakatifu: Roho wa Mungu ambaye anataka kuishi ndani ya wanaomfuata Yesu (ukurasa wa 58).

Shetani: Adui wa Mungu na wana-damu asiyeonekana. (Pia anajuli-kana kama Mwovu).


Ufalme wa Mungu: Ufalme wa Mun-gu upo pale ambapo watu wanamtii.

Ufufuo: Yesu alifufuka katika wafu. Siku moja watu wote watafufuliwa katika wafu. Kisha Mungu atamuhukumu kila mwanadamu (ukurasa wa 53-57).

Ushirika: Wafuasi wa Yesu hukum-buka kifo chake na ufufuo kwa mka-te na mvinyo (ukurasa wa 41).

Uzima wa milele: Maisha na Yesu kama Mungu alivyokusudia. Unashinda kifo na hakuna mwisho (ukurasa wa 23, 29-30 na 59).

Yesu: Jina la Mwana wa Mungu, maana yake, 'Mungu anaokoa'.



YESU MASIHA NI NANI?

Yesu aliishi karibu miaka 2,000 iliyopita katika Israeli. Tunamwita 'Yesu Masiha' au 'Yesu Kristo'. Ina maana kuwa ni Mfalme. Si kwamba Mfalme tu. Yesu aliitwa 'Mwana wa Mungu' na pia 'Mwana wa Watu'. Hii ina maana kwamba yeye ni Mungu na mwanadamu. Historia ya maisha ya Yesu imeelezewa ndani ya Biblia. Ni historia kuu kila wakati.

WAKATI WA YESU

Zama zetu zinaanza kwa kuzaliwa kwa Yesu. Watu walisafiri kwa miguu au kwa pundu, ngamia au juu ya farsi. Sehemu kubwa za Ulaya, Mshariki ya Kati, na Kaskazini mwa Afrika ziliikuwa na dola ya Kirumi. Watu wengi hawakujua kusoma na kuan-dika, lakini Wayahudi katika Israeli waliweza. Waliitwa 'watu wa Kitabu'. Mungu anaongea katika Kitabu, katika Biblia. Yeye ni Muumba wa kila kitu na anataka kuwa rafiki ya kila mtu. Yesu alionyesha hilo kwa uwazi sana.





ISRAELI WAKATI WA YESU

Mji mkuu: Yerusalemu

Majimbo: Galilaya, Samaria, Yudea.

Ukubwa: kilometa za mraba 28,000 hivi.


Tabia ya nchi (hali ya hewa): nusutropiki

Siasa: Tangu mwaka 63 kabla ya Kristo
Waisreali walitawaliwa na Warumi.


Serikali: Gavana wa Kirumi, Pontio Pilato, anatawala Israeli. Tiberio, kaisari wa Kirumi, alimtawala.

Dini: Uyahudi. Wayahudi walikuwa na hekalu Yerusalemu. Makuhani hufanya kila aina ya kazi ya dini na kuna walimu (kama vile Mafarisayo) ambao lazima hu-elekeza watu mafundisho ya Biblia.





Lugha: Kiebrania (lugha ya Wayahudi), Kigiriki (lugha ya kimataifa), Kilatini (lugha ya Warumi).



Kwa sababu gani watu wengi wanakusanyika penye mto?



Kaeni tayari,
Ufalme wa Mungu unakuja.





Watu wote humwita mhubiri huyo pale mtoni,
kwa jina la Yohane Mbatizaji...

Mimi siyo kitu.
Ninamtayarishia
mambo yule
atakayekuja
kutujulisha Mungu ni
nani. Atawabatizeni
kwa Roho wa Mungu
na moto wa Mungu.

Kitendo kama hicho,
kitawageuzeni kabisa.

Na baadaye...




Mimi lazima
nibatizwe
nawe.

Wewe fanya tu.
Ndipo tutayatimiza
mapenzi ya Mungu.

Halafu sauti yasikika kutoka
mbinguni...

Naam,
wewe ndiwe
Mwanangu,
ninakupenda
na
ninafurahiwa
nawe.



Baba,
ufalme wako uje
na utakalo lifanyike.



Ni mwanzo wa majira yetu haya
ndipo Yohane Mbatizaji anapowatayarisha
Waisraeli kwa ujio wa Masiha. Wakati huu, Israeli
ni sehemu ndogo tu ya ufalme mkubwa wa Kirumi.

ISRAELI
KAFARNAUMU
GALILAYA

Nazareti
Kana

YERUSALEMU
YUDEA


YORDANI



Wayahudi,
katika nchi ya
Israeli
wanajisikia kuwa
wanyonge na
wenye kuonewa.
Watu
wanautazamia
kwa hamu,
wakati ule
Masiha
atakapokuja. Masiha
huyu, ndiye Mwokozi
ambaye ujio wake
umeahidiwa katika
maandiko ya
Wayahudi. Yeye
ataistawisha haki ya
Mungi.

Pale mtoni Yordani,
Yohane Mbatizaji anamwonyesha Yesu kwa kidole.

Tazama,
Yule ndiye
Mwanakondoo
wa Mungu
aondoaye dhambi



Baada ya ubatizo wake Yesu, Roho
wa Mungu
anamwongoza Yesu jangwani.



Anakaa huko kwa siku 40 kutwa kucha. Anapokuwa
huko, hali chochote. Kutohana na kusali na kufunga,
anapata kuitambua wazi wazi kazi yake.



Ili apate kufaulu, Yesu lazima
audihhirishie ulimwengu
matakwa ya Mungu.
Ni mpango wa Mungu ya kwamba
watu waepukane na tisho la kifo.

Yesu anajaribiwa na Shetani, mtawala wa giza asiyonekana,
anayeutawala ulimwengu kwa kifo na uovu.




Baba.
Nitalifanya
lolote lile
ulitakalo.



Lakini Shetani, mpinzaji wake, anajaribu kumpa
Yesu fikira potofu ili apate kumshawishi
asiitekeleze kazi ya Mungu.

Ikiwa wewe kweli ni Mwana wa
Mungu, basi, yageuze mawe
haya yawe mkate.

Hapana!
Imeandikwa kitabuni:
Mtu hawezu kuishi kwa kula
mkate tu, bali kwanza
anayahitaji maneno
ayanenayo Mungu.




Ikiwa wewe kweli ni Mwana wa
Mungu, thibitisha!
Jitupe chini kutoka kwenye paa
la hekalu. Je, haikuandikwa
ya kwamba malaika
watakuchukua mikononi?

Tazama. Nitakupa
mamlaka yote duniani kama
ukiniinamia na kuniabudu.




Imeandikwa
pia:
Usimjaribu
Mungu.

Ondoka Shetani.
Imeandikwa:
Sharti tumwabudu na
kumtumikia Mungu peke yake.




Baada ya hayo, Shetani
anamwacha Yesu, kwa wakati
huo. Malaika wanakuja
kumsaidia.






Yesu anajawa na Roho
Mtakatifu
anaporudi Galilaya.
Yesu alipata kukua katika
mkoaa huu, wenyewe watu wengi
sana ulioko kaskazini mwa Israeli.
Wakati anaposafiri, watu wengi
hujiunga naye. Wanafikiri na
kujiulizauliza kama Yesu ndiye
Masiha ambaye habari zake
zimeandikwa na manabii...

Inafanyika harusi katika mji wa Kana ulioko kwenye vilima vya Galilaya...




Yesu pia yupo katika sherehe hiyo, pamoja na mama yake, na baadhi ya marafiki zake.





Kafarnaumu ni mji wa wavuvi unaostawi kando kando ya ziwa Galilaya. Hapa ndipo Yesu anapoanza kuzungumza hadharani kuhusu ufalme wa Mungu.



Na hapa ndipo anapowachagua wanafunzi wake wa kwanza.




Petro, tuendeshe mashua hadi kilindini, huko ndiko mkazitupe nyavu zenu.







Bwana, tumejitahidi usiku kucha wala hatukufanikiwa kupata chochote kile.

Lakini kwa kuwa wewe umesema hivyo...



Ajabu. Sielewi kabisa.






Yesu anazitembelea sehemu zote za Galilaya pamoja na wanafunzi wake.


Anawafundisha watu wote kuhusu ufalme wa Mungu. Anaponya aina zote za maradhi na kuafukuza pepo wabaya.

Watu wanastaajabu na kumfuata. Wengine wanatoka hata kwenye mikoa mingine na Yerusalem, mji mkuu wa Israeli.


Wanalisikiliza, kwa makini, kila neno analolisema.




Heri walio maskini, maana Ufalme wa mbinguni ni wao.



Heri walio na njaa, maana watashibishwa.



Heri walio na huzuni maana watafarijwa.





Heri yenu nyinyi mnapochukiwa na watu kwa sababu yangu.

Furahini na kushangilia maana tuzo lenu ni kubwa mbinguni.

Watendeeni watu wengine
yale mnayotaka
wao wawatendeey nyinyi.

Wapendeni maadui zenu
na kuwaombea.



Tendeni mema faraghani
bila kujionyesha mbele za watu.




Yeyote yule amtazamaye
mwanamke akiwa na shauku
ya kumpata, amekwisha zini
naye moyoni mwake.

Jicho ni taa ya mwili.
Ikiwa jicho lako ni zima,
basi, mwili wako mzima
utakuwa katika mwanga.
Lakini kama jicho lako ni bovu
utaishi gizani.

Hapana mtu awezaye
kuwatumikia mabwana wawili,
au unamtumikia Mungu, au
unaitumikia mali.




Msiwe na wasiwasi kuhusu
kesho. Kwanza utafuteni
ufalme wa Mungu na halafu
mambo mengine yatafuata.



Yatekelezeni haya ninayowaambieni.
Ndipo mtafanana na mtu yule
aijengaye nyumba yake juu ya mwamba.
Msipotekelezeni ndipo mtafanana na mtu ambaye
anajenga nyumba yake juu ya mchanga.


Siku moja makundi ya watu walipokuwa wakisongana kwenye nyumba alimokuwamo Yesu katika mji wa Kafarnaumu...

Hatutaweza kamwe
kuingia ndani humo.



Kuna nini huko
juu?

Waacheni!
Marafiki hao
wana imani kubwa.




Anawezaje huyu kusema
hivyo?


Lipi lililo jambo rahisi zaidi
kumwambia mtu aliye pooza:
'Umesamehewa dhambi'
au 'Simama'.


Anamkufuru
Mungu.

Mungu peke yake ndiye
awezaye kuondoa dhambi.



Masiha anayo mamlaka
ya kuondoa dhambi
lakini, pia ninasema: Chukua
godoro lako na utembee.










Lakini siyo wote wanayafurahia hayo matendo mema ya Yesu.





Viongozi wa dini wanachunguza kama Yesu anazifuata kanuni za sabato.





Katika nchi ya Israeli, watu wanakatazwa kabisa kufanya kazi, ya aina yoyote, katika siku kama hii.










Msongamano wa watu unapozidi, Yesu anaondoka na wanafunzi wake, na kusafiri kwa mashua katika ziwa Galilaya.













Ninawaambieni: Mwana
hawezি kulifanya jambo
lolote ye ye peke yake.
Analifanya lile tu
ambalo alitakalo Baba. Sitaki
kufanya nitakalo, bali mapenzi ya
Baba yangu.
Yeye ndye aliyenituma mimi.




Kwa desturi, Yesu huenda kusali
mahali palipotulia.




Baada ya kusali usiku kucha
Yesu anawateua mitume
wake 12.
Anawatuma wawili - wawili.


Anawapa mamlaka
juu ya pepo wote wachafu
na pia kuponya wagonjwa.



Hawa ndio ndugu wawili
Petro na Andrea...




Ndugu wawili hawa
Yakobo na Yohane...




Filipo na Natanieli...


Toma na Matayo (ambaye hapo kwanza alikuwa mtoza ushuru kwa ajili ya serikali ya Kirumi).



Tadayo na Yakobo mwagine.



Simoni (mpinzani shupavu) na Yuda Iskarioti.




Nendeni, yeote anayewapokea nyinyi, ananipokea mimi, na yeote anipokeaye mimi, anampokea yule aliyenituma.



Hawa mitume 12 wanarudi wakiwa na hamasa kubwa kuhusu kazi yao ya kitume.


Baada ya haya, Yesu anataka kwenda nao mahali pa faragha, lakini makundi ya watu hawakutaka kabisa kuwaachilia.

Mavuno ni mengi, lakini wavunaji ni wachache. Mwombeni yule Bwana mwenye shamba, ili awatume wavunaji wengi wapate kuyavuna mavuno.



Yesu anaendelea tena kuhubiri na kuwaponya wagonjwa. Sasa kunakucha...


Filipo, watu hawa wote watapataje chakula? Tafadhalii wapeni ninyi chakula chochote, wale.



Mshahara wa miezi minane haungeelekea kuwatosha watu hawa.



Yupo hapa mtoto mmoja aliye na mikate mitano na samaki wadogo wawili. Hakuna chochote cha ziada.

Waambieni watu wakae katika vikundi vy'a watu hamsini-hamsini.




Yesu anamshukuru Mungu...

Akaendelea tu kugawa mikate na wale samaki.



Maelfu ya watu
wanalishwa wakati
Yesu anakizidisha
chakula hicho...



Huyu, hakika ndiye yule Mashiha
anayetegemewa kuja.


Sharti tumtawaze
ili awe Mfalme.








Haya, angalieni.
Kuna vikapu 12
vilivyoja tele,
vilivybaki.



Wakati umefika watu hawa waende zao. Nyinyi,
pandeni mashua yenu ili mvuke. Mimi ninabaki
hana mlimani kusali.





Kuna watu wanaotaka
kumtawaza
Yesu ili awe mfalme.

Wao wanatumaini ya kwamba
chini ya uongozi wake,
utawala wa Kirumi
utaondolewa.

Kadhalika, nao wapinzani wa
Yesu, wameongezeka.
Wanaendelea
kumlaumu siku zote.
Wanataka
kumchonganisha na watu
na kumwangamiza.

Bwana, ulifika lini
hapa?

Je, mnanitafuta kwa
sababu ya ile mikate
niliyowapeni?




Msishughulike juu ya chakula
ambacho kitaoza, bali tafutemi
chakula chenye uzima wa milele.

Mimi ndimi mkate wa uzima.
Ni mwili wangu ndio
unatolewa kwa ajili ya uzima
wa ulimwengu.

Je, anavezaje mtu huyu
kutupa mwili wake ili tule?

Upuuzi mtupu!



Hebu, twende
zetu.

Huyu anaelekea
kumdanganya kila
mtu.

Je, nanyi pia mwataka
kwenda zenu?



Bwana, tutakwenda kwa
nani? Wewe unayo maneno
yaletayo uzima wa milele.

Upinzani kwa Yesu unaendelea kuongezeka kwa kasi sana.

Anauhama mkoa wa Galilaya, na kuendelea na kazi yake katika sehemu nyingine za Israeli pamoja na kikundi cha wafuasi: wake kwa waume.

GALILAYA

ISRAELI

Baadaye anaondoka kwenda Yerusalemu.

Wanapokuwa safarini...

Watu wanasema mimi ni nani?

Wanasema wewe ni nabii.


Na ninyi, je?

Mwasema mimi ni nani?

Wewe ni Masiha, Mwana wa Mungu aliye hai.

Msimwambie mtu yeote. Masiha hana budi kwenda Yerusalemu kuteswa na kufa. Lakini siku ya tatu atafufuka kutoka kaburini.

Nje ya mji wa Yerusalemu mara kwa mara watu huuawa.
Wanasulubiwa, ambayo ndiyo adhabu ya kifo ya kikatili ya Warumi.



Kama mtu yejote anataka
kuwa mfuasi wangu, lazima
ajikane mwenyewe, auchukue
msalaba wake, na anifuate.




Mtu yejote anayetaka
kuyaokoa maisha yake
mwenyewe, atayapoteza; lakini
anayeyapoteza maisha yake
kwa ajili yangu, atayaokoa.



Huna budi kujua ya kwamba
kuna Mungu mmoja tu.

Jambo liliilo kubwa ni kumpenda Mungu wako kwa
moyo wako wote, na kuwapenda watu wengine
kama vile unavyoipenda wewe mwenyewe.








Nendeni mkajionyeshe kwa makuhanî.




Je, twende kwa kuhani?
Kupimwa?

Je, baada ya hapo,
ndipo tutapona?




?

!




Tazama!
Nimepona!



Tumepona!

Naam!



Aleluya!
Mungu ni mwema.



Watu 10 walitakaswa, sivyo?
Wale tisa wako wapi? Je,
mbona hawakuja kumshukuru
Mungu?




Simama!
Licha ya imani yako kukuponya,
bali pia imekuokoa.

Viongozi wa Wayahudi,
katika Yerusalemu,
wanawatuma vibaraka wao
kwa Yesu, ili wapate
kumpeleleza
anapokuwa akisafiri.

Wao wanazipinga kabisa
hizo huduma zake bora.

Anashirikiana na watu wenye sifa
mbaya kama vile wazinzi, watoza
ushuru wanaowashughulikia Warumi...

Masiha amekuja
kuwatafuta wale
waliopotea
ili apate kuwaokoa.





Kwa sababu Yesu huwaponya
wagonjwa siku ya Sabato...

Pona!

Na watoto anawapenda kwa
namna ya pekee...


Waacheni hao watoto
waje kwangu. Ufalme wa
Mungu ni mali ya watu
walio kama watoto hawa.



Yesu anaitwa kwenda Betania,
kijiji kilicho karibu na
Yerusalem.

Lazaro ni mgonjwa.
Lazaro pamoja na dada zake
wawili, Marta na Maria,
ni marafiki wakubwa wa Yesu.

Yesu anapofika Betania
mara anapata habari
ya kwamba Lazaro alizikwa
siku nne zilizopita...



Bwana, kama ungalikuwa hapa
kaka yangu hangalikufa.

Kaka yako atafufuka, Marta.





Ndiyo najua.
Atafufuka wakati wa ufufuko,
siku ya mwisho.

Mimi ndimi ufufuko
na uzima. Anayeniamini
mimi ataishi. Je, unaamini
hayo Marta?


Ndiyo Bwana. Mimi naamini
kwamba wewe ndiwe Masiha,
Mwana wa Mungu,
yule anayekuja ulimwenguni.

Mmemzika wapi?

Bwana, njoo uone.



Watawala wa Yerusalemu wanaingiwa na wasiwasi zaidi kuhusu Yesu na wafuasi wake.



Huyo mtu anafanya miujiza mingi mno.

Tukiyaacha mambo haya yaendelee,
Warumi watachukua hatua kali.


Watalivunja hekalu letu na kuliangamiza taifa!



Tumieni busara yenu.
Ni heri zaidi kwamba mtu mmoja afe kwa ajili ya taifa,
kuliko nchi nzima iteketezwe.






Hiyo ndiyo
sababu Yesu
sharti auawe.




Tangu wakati huo,
viongozi wa Wayahudi
wakawa wanatafuta
nafasi ya kumkabidhi
Yesu kwa Warumi
ambao ndio peke yao
wenye mamlaka ya kutoa
adhabu ya kifo.


Huko nyuma, inafanywa sherehe huko Betania...








Karibu itafika sikukuu ya Pasaka. Makundi ya watu wanasafiri wakielekea Yerusalemu.




Mjini Yerusalemu, viongozi wanakula njama za kutia nguvuni Yesu. Hata hivyo ye ye anakwenda.





Hekalu lililoko katika mji huo mkuu, ndilo kitovu cha ibada.




Wakati wa sikukuu ya Pasaka, wanakondoo huchinjwa.



Sehemu ya kila mwaniakondoo hutolewa sadaka hekaluni kwa ajili ya watu ili kuwapatanisha na Mungu.




Lakini, sadaka gani ya mwaniakondoo inaweza kweli kwaondolea watu dhambi zao?











Katika uwanja wa hekalu, watu wanajishughulisha na biashara na kubadilishana fedha.




Ghafla, Yesu pia anajitokeza hapo.










Huyo ndiye Yuda, mmojawapo wa wanafunzi wake.



Yesu anazitumia siku zake kabla ya sikukuu ya Pasaka kwa kuhubiria watu hekaluni, ijapokuwa viongozi daima wanajaribu kumwekea vikwazo ili asifanye hivyo.








Nimetamani sana
kula karamu hii ya Pasaka
pamoja nanyi kabla ya kuteswa
kwangu.




Wenye mamlaka huwatawala
watu kwa mabavu, bali nyinyi,
kamwe msifanye hivyo.






Yule mtumishi wa wote ndiye
atakayekuwa kiongozi wenu.



Mimi niko kati yenu kama
mtumishi.







Baadaye, jioni ile, Yesu na wanafunzi wake wanautoka mji. Yuda hayuko pamoja nao...

Mimi ninawaacheni, lakini Baba atawatumieni
Roho Mtakatifu. Huyo atawasaidieni
na atakuwa nanyi daima.

Nyinyi mnajua njia ile
iendayo mahali ninakokwenda.


Mimi ni njia ukweli, na uzima.
Hakuna mtu yejote awezaye
kuja kwa Baba isipokuwa kwa
njia yangu.

Kaeni hapa. Mimi ninakwenda
mbele kidogo kusali.

Baba, kama inawezakana, niondolee
mateso haya.

Lakini isiwe nitakavyo mimi, bali
kama utakavyo wewe.


Mwavezaje nyinyi kulala wakati mgumu kama huu? Haya, amkeni. Yule anayenisaliti tayari amewasili.



Mshikeni yule ninayembusu.



Shikamoo, Mwalimu!



Bwana,
tupigane nao?



Hapana,
acheni.



Yesu anawaruhusu wamchukue.
Wanafunzi wake wanakimbia ovyo.



Yesu anapelekwa kwa Mkuhani Mkuu, aliye mkuu wa viongozi wote wa Wayahudi.
Petro na Yohane wanamfuata kwa mbali.



Petro aingia ndani ya ua wa Kuhani Mkuu.




Je, wewe hukuwa naye?



Acha upuuzi.
Mimi hata simjui
mtu huyo.

Wewe ni mmoja wao au sivyo?




La hasha!
Simjui.


Nina hakika kabisa, wewe
vilevile ulikuwapo pale!
Kwani wewe pia ni
Mgalilaya!




Bwana, sijui
hata unachosema.



Yesu analetwa mbele ya gavana wa kirumi, Pilato.
Viongozi wa Wayahudi wanawachochea watazamaji.
Wanapiga kelele na kutoa mashtaka ya aina mbalimbali.




Wewe unasemaje
kuhusu mashtaka hayo yote?
Je, huna la kujibu?



Je
umefanya
nini?






Mimi
nimikuja
kuushuhudia
ukweli.


Ukweli ndio nini?



Sioni kosa lolote katika mtu
huyu. Ni sikukuu ya Pasaka.
Nitamfungulia nani,
Baraba au Mfalme wa
Wayahudi?







Huko nyuma, Yuda anajuta
kuhusu yale yote ambayo
ameyafanya.

Nimemsaliti mtu
asiye na hatia.

Yatuhusu nini sisi? Hilo ni
shauri lako.

Mimi
nimekosa.




Yesu anasulubiwa kati ya wahalifu
wawili.

Baba, uwasamehe, kwani
hawajui wanaloafanya.

Ilani inaandikwa katika lugha tatu na kuwekwa juu ya msalaba, nayo imeandikwa hivi: "Yesu, Mfalme wa Wayahudi."

Yesu anakataa kinywaji chenyе kuzuia maumivu.

Askari wanazipigia kura nguo zake.




Kama wewe ni
Mwana wa Mungu,
basi, shuka msalabani!

Naam.
Je, hakuwaokoa
watu wengine?



Jiokoe wewe
mwenyewe, na
sisi pia!

Wewe humwogopi Mungu
hata kidogo. Sisi tunayapata
yale tunayostahili, lakini mtu
huyu hakutenda lolote liliilo
baya.





Unikumbuke
wakati unapoingia
katika ufalme wako.

Nakuambia kwa hakika,
leo hii utakuwa
pamoja nami peponi.

Yapata saa sita mchana, jua
likaacha kuangaza. Kila kitu
kikaingia gizani.

Maria, mama wa Yesu,
na mwanafunzi Yohane,
wanasimama karibu ya msalaba.

Sasa nyinyi ni mama
na mwana.



Mungu wangu, Mungu wangu,
mbona umeniacha?

Nina ... kiu.

Baba, mikononi mwako naiweka
roho yangu.



Yame ... timia.




Yesu anakufa saa tisa alasiri.
Askari mmoja anamtobia Yesu ubavuni;
inatoka damu na maji.



Vitabu vinasema: "Aliongozwa kama mwanakondoo kwenda kuchinjwa."


"Alichomwa na kupondwa kwa sababu ya dhambi zetu." Lakini sasa amekufa.

Je, huyo ndiye Masiha aliyetarajiwa kuja au siye?




Haya, twendeni kuomba idhini ya kumzika.


Yosefu wa Arimataya na Nikodemo wanauchukua mwili wa Yesu. Wanaufungia sanda pamoja na manukato, na kuuweka kaburini. Wanaweka jiwe kubwa mlangoni pake.




Baada ya kipindi cha mapumziko cha Pasaka, wanawake kadhaa, wenyewe huzuni kubwa, wanakwenda kwenye lile kaburi.




Jiwe limeviringishwa mbali na kaburi!



Kwa nini mnamtafuta aliye hai kati ya waliokufa? Amefufuka! Nendeni mkawaambie wanafunzi wake.



Kusikia hivi, Petro na Johane wanazitimua mbio kwenda kaburini.






Pametukia nini?



Kaburi ni tupu kabisa!






Mwalimu!

Siku hiyo, wafuasi wawili wa Yesu, wakiwa wamevunjika moyo, wanamkuta mpita-njia, wakawa wanazungumza naye juu ya kuuawa kwa Yesu...

Je, nyinyi kumbe hamyasadiki yale yote yaliyonenwa na manabii?
Je, haikumpasa Masiha kuteswa?
Hayo yote yameandikwa katika Maandiko Matakatifu.



Ghafla, wakati wa chakula, mgeni wao anatoweka...


Lakini, huyo alikuwa Yesu mwenyewe!



Wanaondoka, mara moja, kwenda kuwatafuta wafuasi wengine wa Yesu.

Tumemwona Bwana!

Maria na Petro nao pia wamemwona!




Ghafla...

Nawatakieni amani.



Je, nyinyi hamwamini ya kwamba mimi ndimi?
Itazame mikono na miguu yangu.

Bwana wangu na Mungu wangu!



Yesu anawatokea wafuasi wake kwa siku 40 mfululizo. Hata anajionyesha kwa watu 500 kwa wakati mmoja.

Siku moja, ikawa baadhi ya wanafunzi wanavua samaki katika ziwa la Galilaya...

Je, vijana, mnacho chakula chochote hapa?

La, hatujapata kuvua chochote!

Hebu, zitupeni nyavu zenu upande mwingine wa mashua.

Salala!
Samaki wengi
kwelikweli!

Ni Bwana huyo!

Mwalimu!

Je, ninyi mnakuja kula
nami?

Je, Petro, wewe kweli unanipenda?

Yesu anamwuliza Petro swali kama hilo mara tatu...

Ndiyo, Bwana,
wewe unajua kuwa ninakupenda.

Tunza kondoo wangu.

Nifuate!

Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Nendeni ulimwenguni mkawafanye watu wa mataifa yote kuwa wafuasi. Wabatizeni kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu, na wafundisheni kuyashika maagizo yote niliyowaambieni.

Kumbukeni tu ya kwamba:
Mimi nipo daima pamoja nanyi, kila siku,
mpaka mwisho wa nyakati.

Baada ya maneno haya,
Yesu anaitoka dunia na kuchukuliwa mbinguni.

Lakini pia amesema
ya kwamba atarudi kuwahukumu watu wote...

Yesu ameondoka.
Wafuasi wake wanangoja
mjini Yerusalem, wakisali.

Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu,
anawashukia
na kuingia ndani mwao.

Roho yule yule aliyejekuwamo
ndani ya Yesu, sasa pia anaishi
ndani yao. Anawawezesha kuwa
watu wapya ambao wanatoa
ushahidi thabiti kuhusu Yesu.


Kifo hakikuweza.
kumdhhibit Yesu.

Mungu alimrudishia
uhai wake.
Mungu alimfanya awe
Bwana wa Mabwana.



Wafuasi wa Yesu wanakwenda popote
ulimwenguni licha ya upinzani mkali.

Yesu ni Mwana
wa Mungu!



Habari hiyo njema
ilitangazwa pia
kwa njia ya barua.

Alizichukua dhambi
zetu katika mwili
wake mwenyewe
alipokufa msalabani.

Hiyo ndiyo sababu
tumekufa kwa
dhambi
na tangu sasa
na kuendelea,
tunaweza kuishi
kama vile Mungu
anavyotaka tuishi.





Sasa wafuasi wa Yesu,
popote ulimwenguni,
hukutanika na kusali
pamoja na kusoma Biblia.


Wanaumega mkate
na kupeana kikombe cha divai
ikiwa ni kumbukumbu
ya kifo cha Yesu.

Wanashirikiana upendo wa Mungu,
uliomo ndani ya miyo yao,
na majirani zao.

Yesu amewawezesha watu
kutimiza makusudio ya
Mungu.



Yesu anakupenda!
Umshukuru na
umwabudu.



Mungu anaupenda ulimwengu
kiasi kwamba amemtoa
Mwanae wa pekee.

Yeyote anayemwamini yeye
hataweza tena kupotea,
bali, atakuwa na
uzima wa milele.



BIBLIA

Hadithi ya Yesu ni kumbukumbu katika Biblia. Hakuna kitabu kingine kilichosomwa na kinachosomwa sasa hivi, mara nyingi zaidi kuliko Biblia. Ni kitabu kili-choja vitabu. Illichukua miaka 1500 kuandika hivi vitabu vyote. Biblia ilikamili-ka miaka 1900 iliyopita. Inajumuisha kila aina ya hadithi kuhusu jinsi Mungu alivyojifunua katika maisha ya watu. Hadithi ya Yesu inaonyesha zaidi Mungu ni nani.


HISTORIA YA YESU

Biblia inajumuisha vitabu 4 ambavyo vinaelezea maisha ya Yesu. Vimetajwa kufuata majina ya waandishi. Waandishi wote waliishi wakati wa Yesu.

1. Mathayo - mfuasi wa Yesu. Alifanya kazi kama mkusanya ushuru. Anafafanua jinsi ambavyo Yesu alivyoshughulika na watu wa Israel (Wayahudi).

2. Marko - bado alikuwa ni kijana wakati ambapo Yesu alikuwa akifanya kazi. Aliandika kidogo kabisu kuhusu miujiza aliyoifanya Yesu.

3. Luka - alikuwa daktari. Yeye binafsi hakumjua Yesu. Luka anaelezea jinsi Yesu alivyoshughulika na watu.





4. Yohana - yeye pia alikuwa mfuasi wa Yesu. Yeye anaonyesha hasa Yesu ni nani. Yesu ni Mungu ambaye alikuwa mwanadamu kuwaweka watu huru kutoka katika dhambi.

KUZALIWA KWA YESU


Mama wa Yesu, Maria, alikuwa bado hajaolewa wakati Yesu alipozaliwa. Alikuwa bado bikira. Mpango wa Mungu ulikuwa kwamba Yesu azaliwe. Muujiza ule ultangazwa katika vitabu vya zamani kabla ya wakati wa Yesu. Yesu hakuzaliwa kama shujaa au mtu muhimu. Alizaliwa kwenye zizi la kulia ng'ombe kwa kuwa hapakuwa na nafasi ya chumba.

MIUJIZA YA YESU

Yesu alifanya miujiza mingi. Biblia inataja aliwaponya watu zaidi ya mara 40. Kwa njia ya miujiza, Yesu alionyesha nguvu ya Mungu na upendo wake. Alionyesha kuwa Mungu anataka kuwasaidia watu na kuwafanya wawe na furaha.



KIFO CHA YESU NA UFUFUO WAKE



Kwa nini Yesu alikuwa? Maelezo yametolewa katika Biblia.

Wakati mwingine watu wote tunafanya makosa. Mambo ambayo hayamfurahishi Mungu na kumfanya kuwa na hasira au kusikitika. Mambo hayo huitwa dhambi. Dhambi zote zinaweza kuzuia watu kuwa marafiki wa Mungu. Hiyo ndiyo sababu Yesu alikuja. Kwa kujitoa kwake Yesu alichukua yeze mwenyewe adhabu ya dhambi zetu. Adhabu hiyo ilikuwa ni kifo. Tangu Yesu afe kwa ajili yetu, tunaweza kuwa marafiki tena na Mungu. Lakini tunahitaji kuomba msamaha kwa makosa tuliyofanya.

Yesu alifufuka katika wafu. Mungu alimfanya hai tena. Kwa tendo hili Mungu alituonyesha kwamba yeze ana uwezo zaidi kuliko kifo.

Sasa Yesu anaishi na Mungu. Na kwa kuwa anaishi, kila wakati anaweza kuwa rafiki yetu. Anataka kutusaidia sisi kuishi katika njia ambayo itamfurahisha Mungu.

MAOMBI

Kama ukitubu kwa makosa uliyoyafanya na kama unataka kuwa rafiki wa Mungu, unaweza kuomba maombi kama haya:

"Mungu mwenye upendo, unanipenda.

Ulimtuma Yesu, Mwana wako wa pekee.

Alikufa msalabani kwa makosa yangu yote niliyoyatenda.

Naomba unisamehe kwa makosa niliyoyatenda. Samahani sana, nisamehe.

Asante, kwamba Yesu yupo upande wangu.

Kila wakati nataka niwe mali yako.

Naomba unisaidie niishi maisha yale unayotaka mimi niishi.

Uwe karibu yangu kila wakati.

Asante kwa kujibu maombi yangu.

Wewe unafanya kila unachokiahidi!"

YESU NA WEWE

Hadithi ya Yesu ina mwisho wa wazi. Yesu alikuwa rafiki ya watu wengi sana, mpaka sasa. Dunia imebadili. Watu wengi hawasafiri kwa punda au juu ya farasi lakini wanasaferi kwa gari na ndege. Lakini hii haifanyi kuwa tofauti kwa Yesu. Anaweza kuwa nasi kama ambavyo alikuwa akitembea Israeli. Haonekani lakini yeze ni halisi. Anataka kuwa rafiki yako leo. Msikilize na unaweza kumpenda yeze.

Je, unataka kujua zaidi kuhusu Yesu na maisha yake? Unaweza kufanya yanayofuata:

1. Anza kusoma Biblia wewe mwenyewe

(kwa mfano: anza kusoma kitabu kilichoandikwa na Luka).

2. Anza kuomba

(ongea na Mungu na msikilize yeze - huhitaji kutumia maneno maalumu).

3. Ongea na watu wengine kuhusu Yesu na Biblia.

Yesu anataka wafiasi wake kukutana pamoja na kutiana moyo na kujifunza zaidi kuhusu yeze.

Text and illustrations: Willem de Vink

Copyright © 1993 Stichting Wereldtaal, Houten, The Netherlands. Published in Dutch as "Jezus Messias".

Edition in Swahili© 1998,2016

Digital copyright under the terms of the Creative commons BY-SA licence

All rights of translation, reproduction and adaptation reserved for all countries.

1998 edition available from: TMP Book Department, P.O. Box 550, Tabora, Tanzania.

Available from: IBS, P.O. Box 60595, NAIROBI, KENYA. ISBN 90-6534-028-9

Revised 2015 edition: available only digital.

Worldwide co-edition organised and produced by:

Wycliffe Netherlands

Postbus 150


3970 AD Driebergen

The Netherlands

+31(343)517444

www.wycliffe.nl

e-mail : picturebook@wycliffe.nl



YESU MASIHA Hii ni hadithi ya kweli ya Yesu Masiha. Aliishi Israel kwa miaka 2000 iliyopita. Kila mtu aliyekutana naye alishangazwa. Hakuna mtu aliyefanya kitu ambacho alikifanya. Hakuna mtu aliyesema kitu ambacho alikisema. Miujiza ilifanya pale Yesu alipokuwa. Na aliletu furaha na furaha kwa wote alikaa nao na kwa waliomsikiliza. Ghafla ikaja kuwa mwisho. Maadui wake walikuwa naye kunyongwa. Lakini huo haukuwa mwisho. Soma wewe mwenyewe jinsi ilivyotokea na angalia jinsi hadithi ya Yesu Masiha inavyoendelea.

Lugha: Kiswahili
language: Swahili
ISBN: 978-90-73150-49-2